# SIRI YA KUBADILISHWA YA BIBI ARUSI

*Warumi 12:1-2, Basi, ndugu zangu , nawasihi, kwa huruma zake Mungu, itoeni miili yenu iwe dhabihu iliyo hai, takatifu ya kumpendeza Mungu, ndiyo ibada yenu yenye maana. Wala msiifuatishe namna ya dunia hii, bali mgeuzwe kwa kufanywa upya nia zenu, mpate kujua hakika mapenzi ya Mungu yaliyo mema, ya kumpendeza, na ukamilifu.*

Natusikilize kile Nabii wa Mungu alichonena:
Hicho ndicho sisi sote tunachotaka kufanya ni: msiifuatishe namna ya dunia hii, bali mgeuzwe kwa kufanywa upya nia zenu ili kufanya lile ambalo ni kamilifu na mapenzi ya Mungu yaliyokubaliwa. Sasa kwamba tumeokolewa kama tulivyo na kwamba tumejazwa na Roho Mtakatifu kama tulivyo; sasa tunataka nia iliyokuwa ndani ya Kristo iwe ndani yetu, kwamba tuweze kugeuzwa kutoka hali ya asili ya mambo ya maisha, na kuvutwa ili kufanya mapenzi makamilifu ya Mungu kwa kugeuzwa na Roho wa Mungu kwa Neno lake.

Tunasoma! Msiifuatishe namna ya dunia hii, bali mgeuzwe kwa kufanywa upya nia..” (Warumi 12:2) Mambo yale uliyowazia kwanza kwamba ni ya thamani, yaweke pembeni na ugeuzwe kwenye kitu kingine, kutoka vile ulivyokuwa kwanza, hata kwa ulivyo sasa.

Hili linatokea “ Kwa kufanywa upya nia zetu, mpate kujua… mapenzi ya Mungu yaliyomema, ya kumpendeza na ukamilifu.

Oh, haya ndiyo ambayo sisi sote tunapenda kujua namna ya kufanya. Unaona? Tuko hapa; tunampenda Yeye, ametuokoa sisi, na sasa tunapenda kujua cha kufanya. Na tulikuwa tunajaribu kuchukua hatua asubuhi hii ya leo, kuinuka kiasi kidogo juu. Wakati mwingine tunagonga mambo ambayo. …Unajaribu kuyashikilia kwa muda…. Mpaka uone kile upatacho kutoka hapo kikoje.

Sasa neno “kubadilishwa” nimeliangalia katika kamusi Jana mpaka karibu nipotee njia kujua ni wakati gani ningepaswa kuwa hapa, nilipokuwa ninaangalia somo. Na ni kama hili Neno au somo hili au maandiko. Na katika kamusi inasema kwamba ni” kitu fulani kilichobadilika”. “kitakacho badilishwa, badili, kifanye tofauti na kilivyokuwa” kilikuwa” Tabia yake na kila kitu kimebadilishwa ndani yake”. Kule kubadilisha.



Na mimi nilikuwa nikiwaza asubuhi yaleo katika Mwanzo 1 Nchi ilikuwa ukiwa mtupu tena utupu na giza lilikuwa juu ya nchi., hakuna chochote isipokuwa ukiwa mtupu.

Na Dunia hii ilipokuwa kwenye hali hiyo, Roho ya Mungu ikatembea juu ya uso wa maji, na picha yote ilibadilishwa kutoka ukiwa utupu na kuwa Bustani ya Edeni. Ile nguvu ya kugeuza ya Mungu, ambayo ingechukua kitu fulani ambacho siyo chochote na kufanya kitu fulani cha ajabu kutoka hicho, hiyo ni nguvu ya Mungu ya kugeuza.

Na Mungu akachukua ukiwa mkubwa wa giza na kuubadilisha kuwa Bustani ya Edeni kwa Neno lake. Hivyo ndivyo tunavyogeuzwa kwa Neno la Mungu. Wakati Mungu aliposema “ Iwepo Nuru” na Bonge hilo la Uumbaji pale likaja juu karibu na jua, na kuanza kuzunguka jua, na ikawa Bustani ya Edeni kwa sababu ilitii Neno la Mungu. Ilifanya mapenzi makamilifu ya Mungu, kwa maana ilibadilishwa kutoka ukiwa na kuwa Bustani ya Edeni kwa Neno la Mungu.

Sasa, Mungu, katika miaka elfu sita amepanda mbegu hizi zote kiajabu au alinena Neno lake “Itakuwa hivi, mti huu utakuwepo, hiki kitakuwepo. Kilakitu kilikuwa kikamilifu. Kilikuwa kizuri. Naye aliamrisha kila kimoja ya hizi mbegu kwamba zingekuwa, zingejibadilisha zenyewe kuwa miti ambayo aina ya uhai wake ni ile ambayo Mungu amenena iwe ndani yao. Kama alivyotaka iwe. Kama ni mti wa mbao ngumu, itoe mti wa mbao ngumu, kama mtende inabidi itoe mti wa mtende.

Kwa sababu Muumbaji mkuu amelituma Neno lake, na lile Neno mbegu lilikuwa pale kabla ile mbegu halisi haijatengenezwa. Na lile neno likaitengeneza ile mbegu. Unaona, Aliiumba dunia kutoka vitu ambavyo havionekani (Waebr.11:3). Unaona, Aliumba dunia kwa Neno lake. Mungu alinena kila kitu kikawepo.

Na yeye akiwa ni Mungu muumbaji alinena vitu vyote vikawepo, ni lazima ilikuwa ni Dunia kamilifu. Ilikuwa ni mahali pazuri pa kupendeza. Ilikuwa ni Paradiso halisi ya hapa Duniani.

Na kila kitu kilikuwa chini ya mamlaka ili kuzaa kwa jinsi yake…. Sasa kumbuka, kuzaa… wakati alipoweka mbegu Duniani, mbegu ingeweza tu kukua kwa nguvu ya uhai ulio ndani yake wa kuigeuza kutoka mbegu kuwa mti, au chochote ilichokuwa. Nguvu yake ya kubadilisha sasa Mungu aliweka zile mbegu pale zikiwa na uwezo kuwa vile alivyosema zitakuwa.

Na ili mradi zilikaa katika kundi sahihi, zingekuwa hasa vile Mungu alisema zitakuwa. Ilipasa iwe hivyo. Kwa sababu aliifanya hivyo na akatengeneza njia yake, mstari wake wa Neno. Itazaa tu hasa kama vile ambavyo Neno lake limesema itakuwa. Haiwezi kuondoka kutoka hapo, imeelekezwa tu kwa usahihi kabisa. Kwa hiyo pamoja na kila kitu alikitumainisha katika Mwana wake, kwamba itakuwa hivyo, Ndipo Mungu akasema. Kila kitu ni chema sana. Kwa hiyo nitaamua nipumzike (Mwanzo 1:31:2:1-3). Na kila moja ya hizi mbegu ilikuwa na uwezo ndani yake wa kujibadilisha yenyewe huwa aina ambayo ilitakiwa iwe. Hivyo ndivyo ilipasa iwe, Kwa sababu nimeipa kila mbegu nguvu ya kugeuzwa ili ije kwenye hali niliyotaka yenyewe kuwa vile hasa mimi ninataka iwe.

Sasa mara nyingine tena Nguvu hii ya kugeuza ni nini? Ni kwa jinsi gani tunaipata? Nguvu hii ya kugeuza inafanya vipi? Mungu anatenda hilo kwa Roho wa Neno lake(Yohana 6:63). Yeye anageuza. Yeye anapanda mbegu zake, anamrusha Roho wake juu ya hilo. Na inaleta matokeo yaliyokusudiwa Roho Mtakatifu wake anageuza mbegu Neno kuwa thibitisho la kilichokusudiwa kwa aina yake.

Wewe ni mbegu gani uliyo, hilo linaonyesha kile ulicho ndani yako. Huwezi ukalificha kile ulicho ndani, kinaonyesha nje. Huwezi ukazuia hicho. Huwezi ukaufanya mti chochote ila kile ulicho. Unaona. Itaenda kuwa hivyo. Roho Mtakatifu anabadilisha, mbegu kule ndani. Haijalishi ni mbegu aina gani. Itabadilishwa hiyo. Kama ni ovu itazaa ovu kama ni Nafiki, itazaa nafiki. Kama ni Neno halisi la Mungu, itazaa Mwana na binti wa Mungu aliye halisi, kupitia chujio la mtu mwenye busara. Ndipo mbegu zinapokua inapopitia hilo; Inazaa mwana na binti wa Mungu.

Na mambo haya yote makuu ambayo alijua yatakuja kutokea, baada ya kuwa amelinena hilo, angelichukua mapunziko. Kila kitu kiko chini ya mamlaka… zake zilikuwa Neno lake, na Neno lake ni Mbegu (Luka 8:11). Yesu alisema lilikuwa. Na kila kitu kingekuwa sawa tu, kwa sababu amesema kuhusu hicho kuzaa kwa jinsi yake vilibadilishwa tu kwa aina yake. Unaona? Neno lake inabidi liwe la aina yake (Mwanzo 1:11-12) kama alisema mti wa mtende, hakumaanisha mtende na mti wa mbao vichangaywe pamoja. Alimaanisha mti wa mtende hapa na mti wa mbao hapa, kila kitu kusimama mahali pake.

Oh kama tu tungeweza kujifunza hilo, kwamba sisi ni sehemu gani ya Neno, lazima tuchukue nafasi zetu, haijalishi ikoje (Ikor 12:18,28-30).



Mara nyingine inabidi utengane na vile uvipendavyo hapa duniani ili kuchukua nafasi yako ambayo Mungu amekuitia. Nina uhakika mnaweza kusoma katikati ya mistari, kile ninachojaribu kusema, unaona? Wakati mwingine mtu yule umpendaye sana duniani, inabidi upeane mikono nao kuchukua nafasi yako ndani ya Kristo kufika pale Mungu alipokuita wewe unaona? Lakini Mungu anafanya nini? Kukugeuza kutoka ulivyokuwa. Pengine binti au mwana ua chochote kile kiwacho wakati mwingine kutoka kwenye nyumba ya mapendano, ana kuweka mahali pengine tofauti, kwa sababu hiyo ni njia yake yakufanya vitu, kwa kufanywa upya nia zenu (waef 4:17-24) kutii Neno la Mungu, bila kujali gharama yake. Unaona Mambo haya hayaji…… hayakutuita……

Wokovu wetu haukuwa kitu rahisi, ilikuwa Mwana wa Mungu afe kwa ajili yetu. Vitu vya thamani huja kwa gharama kubwa (Ipetro 1:17-20).

Neno la Mungu ni Roho wake (Yohana 6:63), na Neno lake linakuja kwa Manabii. Na Neno limekusudiwa likubadilishe wewe kutoka kwenye mambo ya dunia yalivyo, kuja kuchukua sura ya Mwana na binti wa Mungu (Warumi 8,28-27) na neno linaweza tu kuja kupitia hawa manabii kama walivyo nena (Amos 3:6-7). Na inabidi tu ilingane na Neno na kuonyesha kwamba ilikuwa Neno. Sasa kama unalikubali Neno, litakugeuza wewe kutoka mwana wa dunia, binti wa dunia kuwa mwana na binti wa Mungu (Iwathesalonike 1:4-6).

Angalieni ninyi mlio hapa. Ni wangapi hapa walio na ujuzi huo? Kila mmoja wetu. Tumekuwa na ujuzi huo. Kwa sababu ili nenwa; ikaaminiwa; na Neno likaja na kuangukia kwenye udongo wa moyo (Matayo 13:23); na hapo ikakua moja kwa moja kutoka hiyo unaona?

Kujibadilisha wewe mwenyewe, Roho wake Mtakatifu amebadilisha Neno mbegu lije katika sura yake (Warumi 8:28-30, Tito 3:4-7) kama vile mti wa mpera unavyozaa, mapera, kama vile mti wa matofaa unavyozaa matofaa, mambo kama hayo, Neno lake litazaa Wana na Binti za Mungu. Hivyo ndivyo lipaswavyo kufanya.

Siku moja dunia ilipokuwa katika giza na ukiwa tena, Roho wa Mungu alitembea juu ya ile mbegu iliyokusudiwa. Mbegu iliyokusudiwa, iliyokusudiwa, ilibadilishwa. Ilichukua Isaya 9:6-7.

Na hapa, mtu huyu inabidi asimame mbele ya watu na kusema, “Bikira atachukua mimba (Isaya 7:14) oh, inaonekana siyo cha busara…… lakini, unaona, Mungu hakulizungumza mwenyewe; alizungumza hilo kupitia

Manabii. Sasa hakukuwa na chochote kilichoandikwa katika Biblia juu ya hilo, lakini nabii huyu alisimama na kusema "Bikira atachukua……" katika Isaya 9:6," kwa ajili yetu mtoto amezaliwa, tumepewa mtoto mwanamume jina lake ataitwa mshauri wa ajabu, Mungu mwenye nguvu, mfalme wa amani Baba wa milele". Sasa,, kama bikira atachukua mimba hilo neno limenenwa ambalo lilikuwa chembe ya uhai, udongo unabidi uwe pale kulipokea hilo siku moja. Alitafuta katika nchi, hakukuwa na yoyote , Alienda katika nchi hakukuwa na yoyote. Na karibu miaka mia nane baadaye, ile mbegu iliyokusudiwa ilipata udongo, na ikaanza kukua.

Na Roho alitembea ndani ya Yesu na akamtuma msalabani (Yohana 19:17:30) kuleta nuru katika siku yetu, na nuru kwa wote walio mbegu iliyoteuliwa kwa kanisa la leo. Kuwabadilisha wana na binti za Mungu kuwaleta uweponi pake.

Kama unaamini ujumbe wa Biblia, na ujumbe wa sasa wa siku ya leo, na uthibitisho wake…. Sababu inayokufanya ukae hapa, kwa sababu uliteuliwa kimbele kukaa hapa usingekuwa hapa kama siyo hivyo. Ungekuwa kule mitaani, pengine mlevi, baadhi yenu , na wengine wenu nje kule na mkitembea na wanawake wa waume wengine, nanyi wanawake nje kule mmeolewa na mnatembe na waume wa wanawake wengine au kitu kama hicho. Unaona? Lakini mlikuwa mmeteuliwa kimbele kuwa hapa. Unaona? Huwezi kujisaidia. Una Baba, yeye ni Mungu nawe ulikuwa ni mbegu (Mathayo 13:37-38).

Ulikuwa ndani yake kama wazo; sasa wewe ni mtu unayeweza kufanya ushirika naye. Unaona? Kama ulivyokuwa ndani ya baba pale mwanzoni, lakini sasa ninyi ni wana na binti, kwa hiyo unaweza kuwa na ushirika pamoja na wazazi wako. Sasa, tu wana na binti za Mungu, wanaoweza kuwa na ushirika na Baba yetu, Mungu, unaona, ni nzuri. Je hulipendi hilo? Sasa unakuwa kama yeye na kama tu wana tunakuwa sehemu yake na tulikuwa katika sura yake pale Mwanzo.

Na, kumbuka, kama ulikuwa ndani yake pale mwanzo; na wakati Yesu ambaye ni Mungu alipofanyika mwili na akakaa kwetu (Yohana 1:1-3/4) hapo alikuwa ndani yake na ukastahimili matukano aliyoyachukua. ulienda msalabani pamoja naye, ndani yake ulikufa ndani yake. Ulifufuka ndani yake . Na sasa umeketi pamoja naye katika Ulimwengu wa Roho (mbinguni) ndani yake. (waefeso 2:4-6).



Na kutoka kwenye machafuko haya ya Edeni ya Sayansi ya kileo ambayo tunaishi ndani yake katika ustaarabu na sayansi na Elimu na Mambo haya yote ya Kisasa. Tutainuka (tutafufuka) vazi hili mwili wa nyama litadondoka, na kuinuka na kuchukua taji ile ya milele". Siku moja tutapita hewani, na haya yote yatakuwa yameisha (Iwathesalonike 4:13-17) kwa maana Neno la Mungu lilitutoa sisi kutoka kwenye mawazo yetu ya kisasa na nia zetu, kwa kubadilishwa nia zetu na kufanywa wapya mioyoni mwetu kumuelekea Mungu (Waefeso 4:20-24) na roho zetu, roho yule yule Roho aliyenena hilo, ametubadilisha mpaka hapa, na pia atatuchukua sisi mpaka uweponi pake, katika utukufu wake na mwili uliotukuzwa (Warumi 6:5- 6).

Mara moja tena; sasa, kama wewe ni mwana na binti wa Mungu, wewe ulikuwa ndani ya Mungu, wewe ulikuwa ndani ya Mungu tangu mwanzo. Wewe ni sifa zake (Wagalatia 4:6) kama hukuwepo pale basi hukuwepo au hutakuwepo.

Wana na binti walikuwa ndani ya Mungu pale Mwanzo sasa, angalia, wewe unao uzima wa milele (Yohana 5:24) unasema. Tunaliamini hilo, kwamba tunao uzima wa milele. Vyema, kuna aina moja tu ya uzima wa milele na huo uzima wa milele ni Mungu. Hicho ndicho kitupekee kilicho cha milele ni Mungu. Basi kama unao uzima wa milele, uhai huo ulio ndani yako siku zote ulikuwepo, na ulikuwa katika viuno vya Mungu kabla haijakuwepo dunia (Waefeso 1:3-4) Yesu mwenyewe anaitwa Neno, na Yohana 1 alisema"Hapo mwanzo kulikuwepo neno na Neno alikuwa na Mungu na Neno alikuwa Mungu. Na Neno alifanyika mwili naye alikaa kwetu (Yohana 1: 1 –3, 14-18). Hivyo ulikuwa katika viuno vya Yesu, nawe ulienda msalabani pamoja naye. Ulikufa pamoja naye na ulifufuka pamoja naye (Warumi 6:4:-6) na leo tumeketi pamoja naye katika ulimwengu wa Kiroho, tukiwa tumejazwa na Roho wake, wana na binti za Mungu. Kufa pamoja, kufufuka pamoja naye. Kweli.

Sasa unaweza ukawa na Ushirika Naye. Pale nyuma usingeweza kwa sababu ulikuwa ni Neno ndani yake. Mbegu. Lakini sasa amekudhihirisha wewe, na sasa anakutaka wewe uwe na ushirika naye. Ndipo akashuka chini, akafanyika mwili ili aweze kuwa na ushirika mkamilifu na wewe. Unaona ushirika mkamilifu? Oh jamani siri hizi za kindani za Mungu, ilivyo ajabu. Unaona, Mungu asingeweza kuwa na ushirika katika Roho, hivyo Mungu akawa mtu pamoja nasi.

Yesu Kristo alikuwa ni Mungu mwenyewe akidhihirishwa (Warumi 9:5) kwa sababu, yeye alikuwa ni Mwana pekee, lakini ilikuwa ni maskani tu Mungu aliyoishi ndani yake" Hakuna mtu aliyemwona Mungu. wakati wowote, bali Mwana pekee aliyekifuani kwa Baba, huyu ndiye aliyemfunua. (Yohana 1:18) Mungu alijijengea mwenyewe nyumba, mwili wa kuishi ndani yake. Akashuka chini ili tuweze kumgusa ITimotheo 3:16" Bila shaka siri ya utauwa ni kuu Mungu alidhihirishwa katika mwili akajulikana kuwa na haki katika roho, akaonekana na Malaika, akaaminiwa akapokewa juu Mbinguni".

Wewe ukiwa katika mwili na yeye alikuwa ni mwili, hapo sasa mnaweza kuwa na ushirika mmoja naye, kwa sababu alikuwa sifa ya Mungu ya upendo. Mungu ni upendo (1Yohana 4:16). Hivyo ni kweli? Na Yesu alikuwa sifa ya Mungu ya upendo. Na sifa ya Upendo ilipodhihirishwa ambayo ilikuwa ni Mungu mwenyewe, sifa zote zilizoning'inia juu yake zilikuja kwake" wote alionipa baba watakuja kwangu" (Yohana 6:37-44). Hakika walikuwa wamechaguliwa kimbele. Kama isingekuwa hivyo, hungekuwa pale. Ndivyo hasa kwa uhakika.

Sasa tunaweza kuwa na ushirika, kupitia utajiri wa neno lake, ambalo tu sehemu yake. Wewe u sehemu ya Neno; kwa sababu yeye alikuwa neno pale mwanzoni ; wewe ni neno sasa.

Waamini wa kweli waliochaguliwa kimbele watakaa na neno kwa sababu wao ni sehemu ya lile neno.

Sikiliza kuna kitu kimoja siwezi kufanya. Siwezi kujisifu kuhusu wazee wangu wa zamani alisema ndugu Branham. Lakini, ndugu, kuna jambo moja ninaloweza kujisifu juu yake, ninaweza kujisifu juu ya Bwana Yesu. Ambaye ameniokoa mimi. Na kwa nguvu zake za kubadilisha alipanda mbegu kwa uteule wa kimbele, na nikaiona hiyo, ambaye sasa hivi mimi ni mwana wake. Ndiyo naweza kujisifu juu yake. Na nimetumia miaka thelathini na mitatu ya maisha yangu nikimsifia yeye. Kama atanihifadhi mimi miaka mingine thelathini na tatu, nitajitahidi kumsifu yeye zaidi. Unaona? Ninaweza kujisifu juu ya wazee wangu wa zamani (Halleluya). Yeye ambaye ameniokoa mimi na akapanda mbegu ya uzima ndani hapa, na kuniacha niangalie chini hapa katika neno, amemtuma Roho wake hapa chini na kusema. ," liko hapa chini na kusema", liko hapa, sema hili; litatokea. Fanya hivi'. Na oh, mimi, naweza kujisifu juu yake. Amelifanyaje hilo? Kwa kuoshwa kwa maji katika neno, maji ya farakano, natamani Kama ningeweza kulielezea hilo (waefeso 5:25-27).



Anatamani sana kuwa na ushirika na wewe. Anashauku na wewe. Anataka kukubadilisha wewe kwa kufanywa upya nia yako, sio kwa kanisa au kwa dhehebu, lakini kwa Neno lake, ambalo wewe ni sehemu yake kama hiyo njaa iko ndani yako wamebarikiwa wenye njaa na kiu ya haki maana hao watashibishwa (Mathayo 5:6).

Na ametuma nguvu yake ya kubadilishwa ili kukutoa wewe utoke katika uharibifu huu wa dini ambao uko ndani yake. Katika uharibifu huu wa machafuko ambayo tuko ndani, Mungu ametuma nguvu yake yakubadilisha, neno lake, lililothibitishwa, limehakikishwa kukutoa utoke katika uharibifu huu na ujinga wa kidini ambao unatembea ndani yake"uchi, kipofu, mnyonge nawe hujui" ufunuo 3:15-18 fikiria hilo marafiki.

Utukufu kwa Mungu. Hilo linanifanya nijisikie vizuri sana, Unaona? Haijalishi nilivyokuwa; haijalishi nilivyo kuja hapa, tunaweza kubadilishwa na kuipokea ahadi ya siku ya leo, tunapoweza kukaa pamoja kwa umoja na uzuri wa Roho Mtakatifu, na kuishi kama Wakaka na Wadada.

Na kile Mungu alichoahidi kufanya hicho atafanya. Hakuna chochote, kilichopotoshwa Mungu hawezi kushughulika nacho. Lakini yeye atalishika Neno lake, na atamtuma Roho wake, mimi niliyelipanda. Nitalinywesha usiku na mchana. (Isaya 44:3-4) mtu asije akalitwaa mkononi mwangu (Yohana 10:27:29) Biblia ilisema hivyo.

Mungu alisema, yeye atakayemwacha Baba yake, mama, mke na mume, nyumba na mashamba nitawapa nyumba na mashamba, nitawapa baba na mama na Wakaka na Wadada katika ulimwengu huu na uzima wa milele katika Ulimwengu ujao" (Marko 10:29-30).Ni ahadi marafiki. Kwamba Oh hilo inabidi linyweshwe. Kila ahadi Mungu aliyoitoa inakuja kutimia. Kila mbegu ya Mungu ni ahadi.

Ndugu Branham aliulizwa aelezee ile siri ya kubadilishwa ya Bibi Arusi.

Unajua, Mungu alituma nguvu yake ya kubadilishwa kutimiza Neno lake, na kubadilisha mwili wote wa Sarah na Ibrahimu: kumbadilisha mtu mzee na mwanamke mzee, kwa sababu aliahidi kwamba angefanya hivyo (Mwanzo 20).

Miili ya Ibrahim na Sarah ilibadilishwa kukutana na hali ya Neno la ahadi, unaona, walikuwa wazee. Ibrahim aliipokea ahadi na Sarah, wakati alipokuwa na miaka sabini na tano, na mkewe miaka sitini na mitano (Mwanzo 15) akiwa amepita umri wake wa kuingia hedhi. Aliishi naye tangu alipokuwa msichana naye alikuwa nusu dada yake. Na ili ile ahadi

itimie miili yao yote ilibidi ibadilishwe kutoka Mwanaume na Mwanamke mzee na kuwa Vijana mwanaume na mwanamke ili kutimiza ahadi ya siku ile.

Ibrahimu, alikuwa anatazamia mtoto wa ahadi aliyeahidiwa kwake (Warumi 4:16-21) je hiyo ni kweli? Na Kanisa linatazamia kumpata mtoto wa ahadi. Bibi arusi (je hiyo ni Sawa?) Bibi arusi anamtazamia mtoto wa ahadi.

Kabla ya mtoto wa ahadi hajaja kwa Sarah na Ibrahimu, miili yao ilibidi ibadilishwe. Je hiyo ni kweli? Yeye Sarah alikuwa mzee sana kuweza kupata mtoto. Kwa hiyo kulitokea nini? Mungu alimbadilisha kuwa mwanamke mdogo (msichana). Na alimfanyia Ibrahim jambo lile lile, kwa sababu alisema mwili wake ulikuwa kama mfu. Unaona? Na ilibidi abadilishe miili yao ili waweze kupokea ahadi ya mtoto.

Na hatuwezi kumpokea mwana wa ahadi ambaye ameahidiwa leo tukiwa katika miili hii tuishiyo, miili hii ni ya dhambi.

Ubongo huu wa kwanza hutawala mwili huu kwa hisi za kuona, kuonja, kugusa, kunusa kusikia na imetufanya sisi wote tuwe kama walio na wasiwasi; tunajiuliza (hoji) na vitu vyote vile, lakini mwili ule mpya, ule unaokuja kutoka kule kuzaliwa mara ya pili (siyo huu wa kwanza umeshapita) ni kile kitu cha ndani kitu fulani ambacho kinaishi. Kila mtu anayeelewa hilo semeni " Amina.

Siyo hii sehemu ya nje ya kuona, kuonja, kugusa, kunusa, na kusikia, siyo hiyo. Hiyo inapaswa kufa na itakufa, lakini sehemu ya ndani yako, hapa chini. Ndani yako ni mtu yule asiyeweza kufa. Unaona? Na huyo mtu ambaye ule uhai mpya unaanza kutoka hapa, kutoka kwenye kuzaliwa kwapili, na inajenga mtu mwingine katika sura ya mtu ambaye uko, kuzunguka maisha hayo. Unalipata?.

Kwa hiyo kimsingi iko hapa, na ni kitu gani? Lile neno lililoahidiwa kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu. Na kuzunguka pale, hii hapa ina eleleza kivuli, na ile utaeleleza watu halisi lile neno unaona? Na kule kubadilishwa kwa Bibi Arusi kutakuwa namna hiyo hiyo.

Lile neno lililo ndani yako, ule mwili utadhihirishwa kuzunguka lile Neno na jambo hilo hilo lililotokea kwa Sarah.



Ule mwili wa uzee aliokuwa nao Sara ule mwili wa kwanza, ilibidi ubadilishwe ili kufanya mtoto azaliwe. Mwili ule wa kizee usingeweza kufanya hivyo. Huu mwili hauwezi kufanya hivyo; kwa hiyo inabidi ubadilishwe kwa namna ile ile ili kumpokea mtoto (Ikor 15:51-54).

Mungu, tubadilishe sisi leo, kwa nguvu zako, kwa kufanya upya nia zetu kugeuka kutoka vitu vidogo vya dunia hii sasa, kwenda kwenye neno la Mungu. Na tunaomba tufanywe wapya kwa nguvu ya Mungu ya kubadilisha kwenye mbegu iliyoko mioyoni mwetu kwamba tuamini, tuwe viumbe waitwao wana na Binti za Mungu. Hayo ni maombi yangu kwako, Baba, kwa ajili ya watu ni katika Jina la Yesu Amina.

Nukuu za Kiingereza
Ile nguvu ya kubadilisha 965-103,m) Aya 39-48,51 73-74,77-78,281-286,290,296-298-316-317,324 Nguvu ya Mungu ya kubadilisha (65-0911) Aya 37-38, 49-51 64,212,227-245,272 Maswali na majibu (64-0830m) Swali No 362. Utaratibu mwenendo na mafundisho uk. 1113

---

Jiwe la kujengea la Kiroho na 139 kutoka neno la saa hii iliyokusanywa na Gerd Rodewald, Friendenstr. 69.D-75328 Schomberg, Germany simu (+49) 72357613 Fax (+49) 72353306

---

Anakuja mmoja na ujumbe ambao ni moja kwa moja ni Biblia na kazi ya haraka itaizunguka dunia. Zile mbegu zitaingizwa katika magazeti na vitu vya kusomea mpaka kila mbegu ya Mungu iliyokusudiwa kimbele imesikia hilo. (ndugu Branham katika mwendo utaratibu na mafundisho uk.724).

*Kwa nakala zaidi za kiingereza au kiswahili Andika kwa:*

*Charles E.Y. Kanju*
*Box 5138, Tanga*
*E-mail: chaelika@Hotmail.com*
*cellphone: 0784 704299*